**HOTUBA YA MHE. CHARLES MAKONGORO NYERERE MKUU WA MKOA WA RUKWA KATIKA KIKAO CHA JUKWAA LA WADAU WA KODI MKOA WA RUKWA KWA MWAKA 2023/24 TAREHE 21 JUNI, 2024.**

- **Mwenyekiti wa CCM Mkoa,**
- **Katibu Tawala wa Mkoa wa Rukwa,**
- **Mjumbe wa Halmashauri kuu ya CCM Taifa,**
- **Meneja wa Mamlaka ya Mapato Mkoa wa Rukwa,**
- **Kamati ya Usalama Mkoa,**
- **Katibu wa CCM Mkoa**
- **Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,**
- **Waheshimiwa Wabunge,**
- **Mstahiki Meya wa Manispaa ya Sumbawanga,**
- **Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri,**
- **Wakurugenzi wa Halmashauri,**
- **Wakuu wa Taasisi za Umma,**
- **Mameneja wa Benki,**
- **Machifu,**
- **Viongozi na Wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato;**
- **Viongozi na Wawakilishi wa vyama na makundi mbalimbali ya Wafanyabiashara Mkoa wa Rukwa;**
- **Wageni waalikwa,**
- **Waandishi wa Habari,**
- **Mabibi na Mabwana.**

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…………………………….!***

Nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema kwa kutuwezesha sisi sote kukutana mahali hapa tukiwa wazima na wenye afya njema. Niwakaribishe wote mliosafiri kutoka Wilaya mbalimbali ndani ya Mkoa wa Rukwa kuhudhuria kikao hiki cha jukwaa la wadau wa kodi Mkoa wa Rukwa kwa mwaka wa fedha 2023/24.

**Ndugu Wajumbe,** Napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati Kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuona umuhimu wa kuandaa kikao hiki. Naomba niwahakikishie kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan** inachukulia kwa uzito mkubwa sana umuhimu wa kikao hiki kwani ninyi wadau wa kodi na wananchi kwa ujumla ndio mnaiwezesha Serikali kutekeleza ilani ya CCM na shughuli zote za maendeleo pamoja na kutoa huduma mbalimbali za kijamii kupitia kodi mnazolipa. Hivyo, napenda kuwapongeza Sana kwa kuchangia maendeleo ya nchi kupitia kodi zenu mbalimbali mnazolipa.

**Ndugu Wajumbe,** Napenda kusema kwa dhati ya moyo wangu kuwa, Mamlaka ya Mapato Tanzania inastahili pongezi za pekee kwa kufuata maagizo na maelekezo ya Serikali ya awamu ya sita, kwa kukusanya kodi kwa weledi, kuwa wasikivu pamoja na kuzungumza na walipakodi juu ya changamoto wanazozipitia ili waweze kulipa kodi zao vizuri pamoja na kuongeza wigo wa kodi. Lakini usikivu huu wa Serikali ya awamu ya sita usiwe chanzo cha Baadhi ya Wafanya biashara kukwepa kodi kwani kodi ni msingi wa Maendeleo.

**Ndugu Wajumbe,**Nampongeza Meneja wa TRA Mkoa wa Rukwa pamoja na timu ya watumishi wote wa TRA, kwa kukusanya kiasi cha shilingi **bilioni 27.36** kati ya lengo la makusanyo ya shilingi **bilioni 24.45** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikiwa ni sawa na ufanisi wa **112%,** na kwa kukusanya shilingi **bilioni 23.98** mpaka sasa kati ya lengo la shilingi **bilioni 24.25** kwa mwaka huu wa fedha 2023/2024 ikiwa ni ufanisi wa **99%**. **Hongereni sana** na hakika mmeiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake bila kutetereka. Pongezi hizi ziamshe ari ya kufanya kazi kwa ufanisi zaidi, msiishie kuvuka malengo ya miezi kadhaa lakini nataka niwape hamasa ya kuvuka lengo la kila mwaka na mimi nafahamu inawezekana. Kinachotakiwa ni kukusanya kodi kwa weledi, uwajibikaji, uadilifu na kujenga mahusiano mazuri na walipakodi. Sambamba na hilo muendelee kutoa elimu ya kutosha kwa walipakodi na wananchi kwa ujumla kuhusu faida na umuhimu wa kodi kwa maendeleo ya nchi.

**Ndugu Wajumbe,** Nchi nyingi duniani zinategemea kodi kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi wake. Nchi yetu ni mojawapo kati ya nchi hizo zinazotegemea kodi kwa ajili ya kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo, mfano kwa mwaka huu wa fedha kati ya bajeti ya Serikali ya **trilioni 44.4**, TRA inategemewa kukusanya na kiasi cha **trilioni 26.7**. Hii ndio sababu kubwa ya kuboresha mara kwa mara mifumo ya ukusanyaji kodi ya TRA ili kuwarahisisishia wafanyabiashara na wananchi kulipa kodi kwa wakati. Kutokana na umuhimu huu, Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri kwa wafanyabiashara wote wakubwa, wa kati pamoja na wadogo kwa lengo la kuongeza mapato, kukuza ajira na kuondoa umasikini. Sote ni mashahidi na tumejionea jinsi makusanyo yalivyoongezeka lakini pia yale mabavu na kufunga biashara yamepungua kwa kiasi kikubwa sana isipokuwa kwa wananchi ambao wanakiuka sheria.

**Ndugu Wajumbe,** Mapato yenye tija ni yale yanayomnufaisha kila mwananchi. Hivyo, ni lazima kulinda mapato kwa kuhakikisha kuwa, tunaziba mianya ya rushwa na kuzingatia maadili ya utumishi wa umma. Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere enzi za uhai wake, aliwahi kusema **Rushwa ni Adui wa Haki** ikiwa na maana kwamba, rushwa huwaneemesha wachache na kuwanyima haki wengine ambao ndio wengi. Meneja wa Mkoa wa TRA ukisaidiana na viongozi wenzako ndani ya Mamlaka msiruhusu watu wachache wakafaidika huku wengine wakikosa haki zao za msingi. Vyombo vya dola vipo, sitaki kuona suala hili linafumbiwa macho kwa pande zote mbili yaani anayepokea rushwa na anayetoa rushwa.

**Ndugu Wajumbe,** Pamoja na pongezi kwa wafanyabiashara wengi walio wema, kumekuwepo na tabia ya baadhi ya wafanyabiashara ambao siyo waaminifu hasa katika suala zima la kutoa risiti sahihi za EFD. Tabia iliyopo sasa hivi ni ama kutoa risiti pungufu ya fedha aliyolipia mnunuzi au kutokutoa kabisa risiti. Baadhi hutumia risiti moja kusindikiza mizigo kutwa nzima kwenda kwa wateja na wengine hutoa risiti kutoka kwenye mashine bandia ambazo haziko kwenye mfumo wa TRA. Jambo hili halikubaliki na ni kosa kisheria. Adhabu zake zipo kwa pande zote mbili yaani asiyetoa risiti na asiyedai risiti. Nichukue fursa hii kuiagiza TRA kuwa wakali zaidi maana utoaji wa risiti za EFD ndio msingi wa kukadiria kodi kwa haki bila kumuonea mlipakodi na bila kuipunja Serikali. Kupitia kikao hiki, natoa rai kwa wafanyabiashara wanaostahili kutoa risiti za EFD kuhakikisha wanatoa risiti kila wanapofanya mauzo na wanunuzi kuhakikisha wanachukua risiti halali kila wanaponunua bidhaa au kupokea huduma mbalimbali.

**Ndugu Wajumbe,** Kuhusu Elimu ya kodi, Naiagiza TRA kuendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ya wafanyabiashara juu ya umuhimu wa kulipa kodi kwa wakati na hiari ikiwa ni pamoja na kusikiliza kero na kutatua changamoto wanazokutana nazo walipakodi katika biashara zao. Vilevile, natoa wito kwa TRA kufanya kazi kwa karibu na walipakodi pamoja na kuwashirikisha katika masuala mbalimbali yanayohusu kodi hususani pale mnapofanya mabadiliko ya sheria za ukusanyaji kodi kwani hawa ndio wadau wenu wakuu.

Taasisi za Serikali, Mashirika, Asasi za Kiraia na viongozi wote katika Sekta Binafsi hakikisheni mnatoa ushirikiano kwa TRA ili waweze kutimiza wajibu wa kukusanya mapato ya Serikali kwa manufaa yetu sote. Maana utekelezaji wa majukumu yenu kwa wananchi na mishahara ya watumishi inatokana na mapato ya kodi. Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, niwaombe viongozi wote wa vyama vya wafanyabiashara Mkoa wa Rukwa kuwa mstari wa mbele kuhamasisha wanachama wao ambao ni wafanyabiashara kulipa kodi kwa hiari tukizingatia kwamba ujenzi wa Mkoa wetu na nchi kwa ujumla ni jukumu la kila Mtanzania na ndio chanzo cha maisha bora kwetu sote.

Mwisho,niwapongeze TRA kwa kuwajali walipakodi na kutoa fursa hii adhimu ya kusamehe riba na adhabu kabla ya mwisho wa mwezi huu. Hii inaonesha jinsi TRA inavyotekeleza maagizo ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kutumia weledi na ridhaa katika utendaji wa majukumu yao. Hivyo basi, nawahimiza wale wote wenye madeni watumie nafasi hii

kufika ofisi za TRA ili waweze kulipa madeni kwa ustawi wa maendeleo ya Taifa letu.

**Mungu ibariki Tanzania**

**Mungu bariki Mkoa wa Rukwa**

**Mungu Ibariki TRA,**

**Asanteni Sana Kwa Kunisikiliza**

Charles Makongoro Nyerere

**MKUU WA MKOA RUKWA**